**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALIMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA**

# MTIHANI WA UTAHAMILIFU KIDATO CHA NNE, 2023

**021 KISWAHILI**

## MAELEZO

1. Karatasi hii ina sehemu **A, B na C.**
2. Jibu maswali **yote** kutoka sehemu **A, B** na chagua maswali **matatu** kutoka sehemu **C.**
3. Zingatia maagizo ya kila sehemu na kila swali.
4. Andika kwa kutumia kalamu ya wino wa bluu au nyeusi.
5. Simu za mkononi na vitu vyote visivyo ruhusiwa kwenye chumba cha mtihani haviruhusiwi.
6. Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa wa karatasi yako ya kujibia.

**SEHEMU A (alama 15)**

**Jibu Maswali yote Katika sehemu hii**

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x) kisha andika herufi ya jibu hilo katika karatasi ya kujibia.

i. Neno lipi kati ya maneno haya linaweza kudokeza hisia za mtenda au mtendwa
   A. Kiunganishi
   B. Kivumishi
   C. Kihisishi
   D. Kielezi
   E. Kiwakilishi

ii. Lahaja ya kimtang'ata huongelewa sehemu gani ya Pwani ya A.Mashariki?
   A. Kaskazini mwa Pwani ya Tanga.
   B. Kisiwa cha Unguja.
   C. Kisiwa cha Mafia.
   D. Pwani ya Somalia
   E. Kisiwa cha Lamu

iii. Kategoria ya kisarufi inayowakilisha wakati katika kitenzi.
   A. Leksimu

B. Kiambishi awali
C. Shina
D. Mtendewa/mtendwa
E. Njeo

iv. Zifuatazo ni dhima za picha na mchoro katika kamusi isipokuwa ipi?
A. Huvuta umakini wa mtumiaji kamusi.
B. Huwawezesha watumiaji kamusi kuunda dhana ya jambo.
C. Maumbo hunata katika kumbukumbu za watumiaji.
D. Huchafua kamusi na kuifanya ichukize kwa watumiaji.
E. Huwawezesha watumiaji kamusi kuona mfanano

v. Ipi ni maana ya nahau "mbiu ya mgambo" kati ya maana hizi hapa chini.
A. Tia aibu
B. Tangazo maalumu
C. Fanya Tashtiti
D. Mluzi wa mgambo
E. Sare za mgambo

vi. Upi ni mzizi wa neno anakula?
A. Kul
B. La
C. L
D. Kula
E. a

vii. "Mama Zita anakuja" Tungo hii ni tata, utata huo umesababishwa na nini?
A. "Msamiati" mama kuwa na maana zaidi ya moja.
B. Matumizi yasiyo kuwa bayana ya viunganishi na vihusishi.
C. Matumizi ya lugha ya kifasihi.
D. Kutozingatia taratibu za uandishi.
E. Kosa la upatanishi wa kisarufi.

viii. Kwa vipi ngonjera ni igizo?
A. Ina urari wa vina na mizani.
B. Inaimbika
C. Inahusu utendaji
D. Hufanyika mbele ya jukwaa
E. Inahusisha wahusika binadamu.

ix. Kifungu cha maneno ambacho hujibu maswali ya ziada kuhusu tendo katika sentensi huitwa. ________________
A. Kiigizi
B. Kirai Nomino
C. Tungo
D. Kirai kielezi
E. Kikundi kivumishi

x. Ili mzungumzaji wa lugha aweze kuwasiliana kwa usahihi anahitaji mambo manne ambayo ni ________________
A. Mahusiano ya wahusika, muundo, mahali, lengo
B. Lengo, mada, mandhari, umbo
C. Mahali, mada, muda, wahusika
D. Mada, mandhari, lengo,uhusiano wa wahusika
E. Maudhui, lengo, mada, maana.

2. Oanisha dhana zilizo katika **orodha A** kwa kuchagua herufi ya dhana husika katika **Orodha B.** kisha andika herufi husika katika karatasi ya majibu.

| | ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|---|
| i. | Hatua ya kwanza ya uchanganuzi wa sentensi | A. Sentensi nyofu |
| ii. | Kanda | B. Ni kipatanisho cha kiarifu |
| iii. | Shamirisho | C. Shule |
| iv. | Mofimu ni kiambishi | D. Kuainisha maneno ya sentensi |
| v. | Wingi wa shule | E. Mashule |
| | | F. Neno tata |
| | | G. Itakaliwa na maneno ya vitenzi |
| | | H. Kuanisha aina ya sentensi |
| | | I. Usemi huu ni sahihi |

**SEHEMU B. (Alama 40)**
**Jibu maswali yote**

3. Uteuzi mzuri wa maneno ni lazima uzingatie unaongea nini unaongea na nani? unaongea **wapi**? Na kwa **nini**? Eleza kwa ufupi hoja nne.
4. Andika methali inayohusiana na mambo yafuatayo.
   i. Vidole vya binadamu
   ii. Ukulima
   iii. Imani ya binadamu kwa Mungu
   **iv.** Ulevi
5. a) Sentensi zifuatazo zinamakosa kisarufi ziandikwe upya kwa usahihi.
   i. Huyu hapaendi ugovi
   ii. Mafanikio alidondoka pale wakati anamkimbia
   iii. Mtoto angepelekwa hospitalini mapema angelipona
   iv. Mzee Peko alichinja mbuzi zake zote

   b) Kwa kutumia mifano, andika miundo mine (4) ya sentensi shurutia.

6. Wewe na msaidizi wako mmehudhuria kikao cha kupanga mahafali ya kumaliza kidato cha nne. Andika kumbukumbu ya kikao kilichofanyika katika shule kilichokuwa na wajumbe nane.
7. Ukuaji na ueneaji wa lugha ya Kiswahili, umepitia vipindi vingi tofauti, fafanua kwa mifano mambo manne (4) yaliosaidia kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili baada ya uhuru.
8. Soma kifungu cha habari kisha jibu maswali yafuatayo:

Nchi ya Tanzania hufanya uchaguzi wake kila baada ya miaka mitano, uchaguzi mkuu huhusisha uchaguzi wa Rais, Wabunge, na Madiwani. Octoba 2020 watanzania wote walikuwa katika pilikapilika za kuwapata viongozi wa kuwawakilisha katika matatizo yao.

Mtanzania aliyekuwa huru kuchagua viongozi wake alitakiwa kutimiza masharti yafuatayo:-
Awe amejiandikisha katika daftari la kudumu la wapiga kura, awe na umri wa miaka kumi na nane na kuendelea, awe raia wa Tanzania na awe na akili timamu.

Uchaguzi ulifanyika kwa amani, wananchi waliweza kuelemishwa kupitia vyombo vya habari kama redio, magazeti, Runinga pamoja na majarida. Kwa kutumia vyombo hivyo vya habari zilifika sehemu zote za nchi yaani mijini na vijijini, kila mtanzania alijua uchaguzi ni muhimu kwake kwani hutupatia viongozi bora kuendeleza demokrasia, kuleta mabadiliko nchini na kutatua migogoro

mbalimabli katika jamii pamoja na kuondoa ubaguzi. Watanzania tushikamane kuendeleza amani nchini.

**MASWALI:**

A. Pendekeza kichwa cha habari kifaacho kwa habari hiyo.
B. Uchaguzi hufanyika kila baada ya miaka mingapi hapa Tanzania?
C. Taja sifa tatu za mtu anaetakiwa kupiga kura.
D. Unafikiri uchaguzi una umuhimu? Kama ndio au hapana toa hoja tatu.

**SEHEMU 'C' Alama (45)**

**Jibu maswali matatu tu kutoka sehemu hii**

9. Umealikwa kwenda kuelimisha jamii yako juu ya "madhara ya mapenzi katka umri mdogo". Tunga mchezo mfupi wa kuigiza usiozidi maneno (300) mia tatu kuhusu mada hiyo.

**ORODHA YA VITABU**

**USHAIRI**

| | | |
|---|---|---|
| Wasakatonge | - | M.S. Khatibu (DUP) |
| Malenga Wapya | - | TAKILUKI (DUP) |
| Mashairi ya Chekacheka | - | T.A Mvungi (EP & DLTP) |

**RIWAYA**

| | | |
|---|---|---|
| Takadini | - | Ben Hanson (M.B. S) |
| Watoto wa Mama Ntilie | - | E. Mbogo (H.P) |
| Joka La Mdimu | - | A.J. Safari (H.P) |

**TAMTHILIA**

| | | |
|---|---|---|
| Orodha | - | Steven Raymond (M.A) |
| Ngoswe penzi kitovu cha uzembe | - | E. Semzaba (E.S.C) |
| Kilio chetu | - | Medical Aid Foundation (F.P.H) |

10. Mashairi siku zote hukemea uonevu katika jamii. Thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja 3 kutoka katika kila diwani kati ya diwani mbili ulizo soma.

11. Kwa kutumia riwaya mbili ulizosoma, fafanua namna ambavyo waaandishi wametumia kipengele cha mtindo kuumba kazi zao. Eleza hoja tatu kwa kila kitabu.

12. Kwa kutumia hoja tatu kutoka kwa kila tamthiliya kutoka katika tamthiliya mbili ulizosoma. Jadili kufaulu kwa mwandishi katika kipengele cha matumizi ya lugha.